BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 02 Juni, 2026

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2026/2027.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Ardhi na Tehama:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Miundombinu, Ardhi na Tehama kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2026/2027.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

241. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Miundombinu ya mitaro, makaro na mabomba ya maji machafu ya baadhi ya mitaa ya jimbo la Malindi ikiwemo Gulioni, Mlandege, Mchangani, Mwembe Tanga na Vikokotoni, imezidiwa kimatumizi na kusababisha kuziba na kufoka kwa maji machafu mitaani.

(a) Je, lini Wizara itakuwa na mpango madhubuti wa kufanya marekebisho ya miundombinu ya mitaro hiyo ya zamani iliyozidiwa kimatumizi.

(b) Je, kuna mkakati gani wa Manispaa ya Mjini kuongezewa uwezo na vifaa vya kusafishia mitaro hiyo kutoka Serikali Kuu.

524. MHESHIMIWA SAID ALI JUMA (Uteuzi wa Rais) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:

Bwawa la Mwanakwerekwe ni miongoni mwa mabwawa makubwa yaliyokuwepo pembezoni mwa barabara na litakuwa na mandhari nzuri ya kuvutia pindi litakapoboreshwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuliboresha Bwawa hilo.

<u>**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**</u>

487. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji

Baadhi ya taasisi hasa za binafsi zinachukulia kawaida sana suala la mikataba kwa watendaji wao jambo ambalo limekuwa ni kero sana kwa watendaji wa taasisi hizo kwa maana mikataba kwao imekuwa ni sawa na mfungo wa njugu haizingatii mjazo wa kipimo wapo wanaopewa mikataba miezi 3, miezi 6 na mwaka mmoja.

(a) Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa taasisi hizo ambazo zinaendelea na mfumo huo.

(b) Je, mkataba ni mali ya nani kati ya muajiri na muajiriwa.

<u>**Wizara ya Fedha na Mipango:**</u>

9. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa kila mwaka, wamiliki wa vyombo vya moto hukata bima kwa vyombo vyao ama ya mtu wa tatu (Third Party) au hata bima kubwa (Comprehensive) kwa lengo la kuwasaidia watumiaji wa vyombo hivyo ikiwa ni pamoja na wananchi kupata fidia wanapopata ajali.

(a) Serikali imefanya juhudi zipi za kuwaelimisha wananchi ili

wafahamu haki zao pale wanapopata ajali barabarani.

(b) Kuna sababu zipi zinazowafanya wananchi wengi kutofuatilia haki zao za bima pale wanapopata ajali na wakawa na haki ya kupata fidia.

(c) Kwa mwaka 2025, ni wananchi wangapi walifuatilia haki zao za fidia za bima baada ya kupata ajali Zanzibar na wangapi wamefanikiwa kupata haki zao.

267. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa miaka mingi, wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba wanapata shida kwa kukosa sehemu sahihi ya kusherehekea skukuu na kulazimika huifuata huduma hiyo Chake Chake jambo linalowakwaza sana watoto na wazee wao.

Ni lini Wizara kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), italipatia ufumbuzi jambo hili kwa kuwajengea Kiwanja cha Kufurahishia Watoto ndani ya Mkoa wa Kaskazini Pemba ili kuondoa usumbufu uliopo sasa.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

171. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali imekuwa na utaratibu wa kuweka nguvu nyingi kwenye majengo mapya ya kufundishia watoto (skuli mpya), badala ya kutazama pia maslahi mapana ya walimu pamoja na watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

(a) Je, ni lini Serikali italipa maposho ya walimu wanaodai malimbikizo yao ya nauli pamoja na likizo.

(b) Kwa nini Serikali haiukamilishi na kuuwasilisha katika Baraza hili Mswada wa Sheria ya Tume ya Utumishi ya Walimu.

(c) Ni lini Serikali itaajiri walimu wapya ili kuondoa changamoto za upungufu wa walimu hasa kwenye Skuli ya Chambani na Ukutini Pemba.

## Wizara ya Afya:

422. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuimarisha huduma za afya kwa wananchi wake katika maeneo tofauti. Hata hivyo, Kituo cha Afya cha Kibondeni kinakabiliwa na changamoto ya kuharibika kwa tanuri za kuchomea taka hatarishi pamoja na uzio jambo ambalo linasababisha moshi na taka hatarishi kuzagaa mitaani na kupelekea athari kwa jamii iliyoizunguka.

Ni lini Serikali itaanza marekebisho ya tanuri hilo lililoharibika kwa zaidi ya miaka mitano sasa pamoja na kuweka uzio.

## Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

483. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Enzi za Serikali ya Awamu ya Kwanza na ya Pili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, masuala ya maadili ya mavazi kwa wageni wanaoingia na kutoka ndani ya Zanzibar yalizingatiwa sana kwa kutakiwa wageni wavae mavazi yanayoendana na maadili ya kizanzibari.

(a) Je, ni ipi hatma ya maadili yetu ya kizanzibari kimavazi kwa wageni wetu wanaoingia nchini kwa sasa.

(b) Serikali inaitathmini vipi athari ya uvunjwaji wa maadili ya kizanzibari kimavazi.

(c) Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na namna wageni wanavyoingia nchini na mavazi yao.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

265. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji,Nishati na Madini:

Katika siku za hivi karibuni kumekuwa na changamoto kubwa ya kukatika umeme pamoja na umeme kuwa mdogo katika maeneo mbalimbali ya kisiwa cha Unguja.

(a) Je, Serikali inawaeleza nini wananchi kuhusiana na changamoto hii.

(b) Serikali ina mikakati gani ya kukabiliana na changamoto hii na lini changamoto hii itapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

114. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Hivi karibuni bidhaa ya chakula ya nyama imepanda bei kwa kiwango kikubwa na kuleta athari kwa watumiaji wa bidhaa hiyo ya chakula.

(a) Je, nini kilichopelekea bidhaa hiyo kupanda bei kwa kiwango kikubwa.

(b) Je, ni hatua gani zimechukuliwa za kurekebisha changamoto za kupanda bei ili kushusha bei hiyo.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

55. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kwa kuwa zoezi la utambuzi na usajili wa ardhi Unguja na Pemba lilianza kutekelezwa kwa kipindi kirefu sasa.

(a) Ni kwa jinsi gani mifumo ya kisasa ya teknolojia imesaidia katika zoezi hili.

(b) Ni kwa jinsi gani zoezi la usajili wa ardhi limewasaidia wananchi kutumia hati zao katika kupata mikopo katika sekta za fedha.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

94. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kumekuwa na changamoto ya kufanyika shughuli za upakiaji na ushushaji wa mizigo katika bandari ya Mkokotoni kutoka na kujaa maji. Wadau wa bandari wameishauri Serikali kuwekeza katika kuisogeza mbele bandari hiyo, ili kufikia kina cha maji ambacho kitawezesha vyombo kufunga na kufanya shughuli zao kwa muda

wote.

(a) Kwa kutambua tatizo hilo, je Serikali ina mpango gani iliouandaa kukabiliana na changamoto hiyo.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kinaweza kuhitajika ili kuondosha changamoto hiyo.

363. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Barababara ya Machui kuelekea Miwani ni miongoni mwa barabara muhimu zinazorahisisha shughuli za wananchi katika maeneo yao hasa shughuli za kiuchumi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga kwa kiwango cha lami barabara hiyo.

## Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

297. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuwa shughuli za uwekezaji zinahitaji vivutio mbalimbali,

(a) Kuna tofauti gani kati ya wawekezaji wanaowekeza katika visiwa vidogo vidogo nchini na wale wanaowekeza katika visiwa vikubwa ikiwa ni pamoja na cha Baramlia.

(b) Je, kodi na malipo ya Serikali yanafanana na kutofautiana vipi kwa wawekezaji hao baina ya visiwa hivyo vidogo na vikubwa.

## Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

141. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kwa kuwa wavuvi wadogo wadogo bado wanakabiliwa na vifaa duni vya uvuvi na masoko ya uhakika.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuwasaidia wavuvi hawa ili kuongeza uzalishaji na kipato chao.

**<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

386. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kulikuwa na mfumo wa marekebisho ya mishahara kwa kuzingatia madaraja ya uzoefu wa kazi kila baada ya miaka 3, ambapo mfanyakazi aliyetimiza miaka 12 alipanda daraja lenye manufaa zaidi.

(a) Kwa kiasi gani Serikali inatambua kuwa mfumo huo haujaendelea.

(b) Je, mfumo huo umefutwa kwa utaratibu wa sheria au kwa utaratibu upi ulio rasmi.

(c) Je, Serikali imejipanga vipi kurekebisha tofauti za mishahara miongoni mwa wafanyakazi wake, msisitizo ukiwekwa kwa walimu.

## III. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

**<u>Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**02 Juni, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**<u>WAWAKILISHI, ZANZIBAR</u>**